TANGAZO LA SERIKALI Na. 110 la tarehe 14/2/2025

SHERIA YA MAMLAKA NA MAJUKUMU YA MSAJILI WA HAZINA
(SURA YA 370)

# HATI YA UHAMISHO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(2))*

HATI YA UHAMISHO WA VIWANJA VINAVYOMILIKIWA NA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA KWENDA KWA JUMUIYA YA KIDINI YA KHOJA SHIA ITHNA ASHERI JAMAAT YA MWAKA 2025

Sura ya 370
Sura ya 257

**KWA KUWA**, kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina ikisomwa pamoja na Sheria ya Mashirika ya Umma, mali zote za Serikali zimewekwa chini ya umiliki wa Msajili wa Hazina;

Sura ya 370

**NA KWA KUWA**, Rais anaweza, chini ya kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, kutoa maelekezo kwa Msajili wa Hazina ya uondoshaji wa mali za uwekezaji au mali nyingine zinazoshikiliwa na Msajili wa Hazina chini ya udhamini, na Msajili wa Hazina atatekeleza maelekezo hayo;

**NA KWA KUWA**, Serikali imeona kuwa inafaa kwamba Viwanja sita vilivyopo eneo la Posta, Wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam, vinavyomilikiwa na Shirika la Nyumba la Taifa, kuhamishwa kwenda kwa Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat kwa kubadilishana na viwanja kumi na tisa vilivyopo katika eneo la Mtoni Kijichi, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam, vinavyomilikiwa na Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat;

**NA KWA KUWA**, viwanja sita vinavyomilikiwa na Shirika la Nyumba la Taifa vina thamani ya Shilingi Bilioni Tisa na Milioni Mia Nne na Hamsini na Nne, na viwanja kumi na tisa

vinavyomilikiwa na Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat vina thamani ya Shilingi Bilioni Mbili Milioni Mia Saba na Themanini na Nne, Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat italipa kiasi cha Shilingi Bilioni Saba na Milioni Mia Tano na Hamsini kwa Shirika la Nyumba la Taifa ikiwa ni nakisi baina ya thamani ya viwanja sita vinavyomilikwa na Shirika la Nyumba la Taifa na thamani ya viwanja kumi na tisa vinavyomilikiwa na Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat;

**HIVYO BASI**, imeelekezwa kama ifuatavyo:

Jina

**1**. Hati hii itajulikana kama Hati ya Uhamisho wa Viwanja Vinavyomilikiwa na Shirika la Nyumba la Taifa Kwenda kwa Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat ya Mwaka 2025.

Uhamishaji wa viwanja

**2**. Viwanja vilivyoainishwa katika Jedwali la Hati hii vinavyomilikiwa na Shirika la Nyumba la Taifa, pasipo hitaji la uthibitisho wa ziada na kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Hati hii, vinahamishwa kwenda kwa Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Mkoa | Hati Na. | Namba na Maelezo ya Kiwanja | Taasisi Inayohamishiwa |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 123 | Kiwanja Na. 518/75 chenye ukubwa wa mita za mraba 765.71 mtaa wa Asia, Posta, Wilaya ya Ilala. | Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat |
| | 2830 | Kiwanja Na. 1662/75 chenye ukubwa wa mita za mraba 141.21, kilichopo mtaa wa Asia/Indira Ghandi, Posta, Wilaya ya Ilala. | Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat |
| | 186016/12 | Kiwanja Na. 2032/73 chenye ukubwa wa mita za mraba 349.04 kilichopo mtaa wa Indira Ghandi, Posta, Wilaya ya Ilala. | Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat |
| | 186005/27 | Kiwanja Na. 678/78 chenye ukubwa wa mita za mraba 322.47, kilichopo mtaa wa Mali, Posta, Wilaya ya Ilala. | Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat |
| | 186016/34 | Kiwanja Na. 2620/73 chenye ukubwa wa mita za mraba 311.19 kilichopo mtaa wa India, Posta, Wilaya ya Ilala. | Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat |
| | 186016/38 | Kiwanja Na. 2099/72 chenye ukubwa wa mita za mraba 177.81 kilichopo mtaa wa India, Posta, Wilaya ya Ilala. | Jumuiya ya Kidini ya Khoja Shia Ithna Asheri Jamaat |

**KWA AMRI YA RAIS**

Dodoma,
………………, 2024

MOSES M. KUSILUKA,
*Katibu Mkuu Kiongozi*